



**Jamhuri ya Muungano wa Tanzania
Wizara ya Mambo ya Katiba na Sheria**



**WAKALA WA USAJILI UFILISI NA UDHAMINI
(RITA)**

TAARIFA KWA UMMA

**KUKANUSHA TAARIFA KUHUSU RITA KUSAJILI BODI MPYA YA
WADHAMINI WA CHAMA CHA WANANCHI (CUF)**

Katika Gazeti la Mtanzania Toleo namba 8494 na Gazeti la Mwananchi Toleo namba 6087 yaliyochapishwa siku ya Jumanne tarehe 28 Machi 2017 yaliandika taarifa kuhusu Wakala wa Usajili Ufilisi na Udhadini (RITA) kusajili Bodi mpya ya Wadhamini wa Chama cha Wananchi (CUF) mnamo tarehe 27 Machi 2017.

RITA inapenda kukanusha taarifa hiyo na kutoa maelezo yafuatayo:

- 1) RITA ni Wakala wa Serikali wenye majukumu ya Kusajili na kutoa hati ya Usajili kwa Wadhamini wa Vyama vya Siasa, Vikundi vya kijamii, Mekanisa, Misikiti, Mifuko ya maendeleo na taasisi nyingine za kijamii zinazomiliki mali. Utekelezaji wa Majukumu haya ni kwa mujibu wa Sheria ya Miunganisho ya Wadhamini SURA YA 318, TOLEO LA 2002.
- 2) RITA hupokea maombi ya kufanya mabadiliko ya wadhamini wa Taasisi ilizozisajili na kuyapitia iwapo yamefanyika kwa mujibu wa Sheria na Katiba za Taasisi husika na ndipo hutoa barua ya kutambua Bodi ya Wadhamini husika. Hii ni kwa mujibu wa Kifungu 16(2) cha sheria husika.
- 3) Tarehe 27 Machi 2017, Wakala ulipokea maombi ya Usajili wa Bodi mpya ya Wadhamini ya CUF. Kwa mujibu wa utaratibu, maombi hayo yakipokelewa hupitia katika hatua ya uchambuzi wa taarifa zilizowasilishwa ili kujiridhisha sababu za mabadiliko hayo, na kuangalia iwapo taratibu zilifuatwa katika upatikanaji wa wadhamini hao kwa kuzingatia maamuzi ya mkutano uliohusika kupitisha mabadiliko hayo hii ni kwa mujibu wa Kifungu 17(1). Hatua hii bado haijakamilika.

RITA inapenda kuufahamisha Umma kwamba hakuna mabadiliko yoyote yaliyoidhinishwa kuhusu Bodi ya Wadhamini ya CUF na maombi yaliyowasilishwa bado yanafanyiwa kazi kwa mujibu wa sheria na taratibu zinavyoelekeza.

**Emmy K. Hudson
Kaimu Afisa Mtendaji Mkuu/ Kaimu Kabidhi Wasii Mkuu**

29 Machi 2017